- Wafundishe tembo kutovamia mazao - tumia njia tofauti kuzuia tembo kuvamia mashambani
- Fikiria jinsi tembo hai, ujuzi wako na uzoefu wa kuishi na tembo vinavyoweza kuleta faida zaidi
- Epuka kuvuka njia za tembo mapema asubuhi (10 alfajiri -2 asubuhi) na jioni (12 jioni- 6 asubuhi), haswa wakati wa kiangazi / msimu wa baridi
- Kumbuka tembo wanafanya kazi zaidi wakati wa usiku
- Usitembee usiku bila tochi

## Mambo 14 kuhusu Tembo

1. Tembo wa Kiafrika ndiye mamalia mkubwa zaidi nchi kavu.
2. Kwa wastan uzito wa tembo mkubwa wa Kiafrika ni Kilogram 6000.
3. Tembo hukua katika maisha yao yote. **Wastani wa urefu wa bega la tembo mkubwa ni mita 3.2.**
4. Kipindi cha ujauzito ni miezi 22. **Ndama aliyezaliwa mchanga huwa na uzito wa Kilogram 120.**
5. **Tembo hula 4% hadi 6% ya uzito wa mwili wake kwa siku.** Tembo hula nyasi na miti.
6. Tembo mkubwa anaweza kunywa maji Lita 200 kwa siku.
7. Tembo anaweza kuishi hadi miaka 60-70.
8. **Uwezo wa kusikia na kunusa ni mkubwa,** uwezo wa kuona ni wa wastani.
9. Pembe ni meno ya juu ambayo hukua katika maisha yote ya tembo.
10. Tembo huishi katika makundi ya familia yanayoongozwa na tembo jike mkongwe anayejulikanaye kama MATRIACH.
11. Tembo dume wafikishapo miaka 12-20 huunda makundi yao yajulikanayo kama kundi la BACHELOR.
12. Idadi ya ndovu nchini **Tanzania inakadiriwa kuwa 50,000.**
13. **Kupitia hisia kali za harufu,** tembo atajua shamba lilipo na anaweza kuvamia mazao.
14. Tembo wasio na pembe ni hatari.


**FOR MORE INFO CONTACT**

Ecoexist Trust
Maun, Botswana
Tel: +267 683 0240 | +267 684 0290
Email: info@ecoexistproject.org
Website: www.ecoexistproject.org


ecoexist



ecoexist

# Field Guide 3

## Kujilinda

Tembo ni wanyama wenye akili na wanafanana na watu kwa njia nyingi. Sisi sote tunahitaji maji, chakula na nafasi ya kuishi. Japokuwa kushiriki nafasi na tembo inaweza kuwa ngumu! Miongozo hii inakusudia kutoa maoni na vidokezo juu ya jinsi tunavyoweza kuishi pamoja kwa amani na kupunguza migogoro inayotokea kati ya watu na tembo.

## Nifanye nini nikimuona tembo?

- Tulia
- Usikimbie
- Subiri tembo aendelee au apite
- Jaribu kuchunguza tabia yake
- Usiangaze tochi / taa mbele ya jicho la tembo
- Umsipige ndovu (isipokuwa kama hakuna chaguo jingine)
- Umsipige changamoto tembo (haswa ikiwa una pombe au dawa za kulevya katika mfumo wako)
- Usipige honi yako au kuendesha kwa fujo kuelekea kwa tembo

## Tabia ya tembo

**Tembo ni mnyama jamii ya herbivora** (huwa wanakula mimea tu) na anaweza kupatikana katika makazi tofauti ikiwa ni pamoja na savanna, misitu, jangwa na sehemu zenye maji. Wanapendelea kukaa karibu na maji. Wanachukuliwa kama spishi za msingi kwa sababu ya athari zao katika mazingira yao.

**Tembo jike** huishi katika makundi ya familia, ambayo yanaweza kuwa na jike na watoto wake au jike kadhaa wenye mahusiano. Makundi yanaongozwa na jike ajulikanaye kama "matriarch", mara nyingi huwa ni mwenye umri mkubwa kuliko wote.

**Madume** huondoka katika makundi yao ya familia wanapofikia, na wanaweza kuishi peke yao au na madume wengine. Madume wakubwa hushirikiana sana na makundi ya familia wakati wanatafuta wenzi na huingia katika hali ya kuongezeka kwa testosterone na uchokozi unaojulikana kama musth, ambayo huwasaidia kutawala na kuzaa kwa mafanikio.

Tembo kwa ujumla ni watulivu, lakini wanaweza kuwa wakali wakati wanapingwa au kuogopa. **Hivyo, mara nyingi hutoa ishara za onyo kabla ya kukasirika / kushambulia.**







## Ishara za Tahadhari ya Tembo

**1. KUTOA MASIKIO**
Ishara ya onyo la kwanza tembo atatoa, ni kusukuma masikio nje

**2. KUTIKISA KICHWA**
Onyo la pili ni kutikisa kichwa

**3. UZALISHAJI KUTOKA KWENYE TEZI**
Tembo wanapokuwa na mafadhaiko huonyesha alama yenye enyevunyevu/nyeusi kati ya sikio na jichoe

## Hasira ya tembo

**1. KUTISHIA KUKASIRIKA**
Mara nyingi, tembo hutishia kukasirika, akipiga kelele na masikio yake nje, ni hasira ya kutishia. Wakati anapotishia kukasirika, tembo anaweza kuanza kuonyesha kutokuwa na uamuzi kwa kurudi nyuma au mbele au kutoa sauti kabla ya hasira ya kweli.

**Nini cha kufanya:**

Usikimbie | Tulia | Piga makofi | Kaa kwenye kikundi | Punga mikono yako hewani na kupiga kelele

**2. HASIRA YA KWELI**
Wakati wa hasira ya kweli, tembo huweka tu kichwa chake chini, masikio yamejaa juu ya kichwa chake na hushambulia bila kusita na mara nyingi bila sauti.

**Nini cha kufanya:**


Ondoka njiani | Toa sauti kubwa kwa ukali | Jaribu kupanda juu - panda kichuguu au mti | Rusha kipande cha nguo na uelekee mwelekeo tofauti

**TEMBO NDUME ALIYE KWENYE KIPINDI CHA KUTAKA JIKE**
Tembo dume aliye kwenye kipindi cha kutaka kupanda anweza kuonyesha dalili fulani kabla ya kushambulia. Ni busara kutosubiri huyu ndovu hata kama mara kwa mara huenda akaondoka bila kuonyesha hasira. Mara nyingi huwa peke yake na hunyanyua kichwa juu. Atakuwa na mabaka makubwa yenye unyevunyevu kati ya macho na masikio. Anaweza kutoa mkojo na atakuwa na harufu kali.

**Nini cha kufanya:**

Kaa mbali | Pita njia nyingine

## Mambo muhimu ya kukumbuka




Mara nyingi mwelekeo wa upepo utakuwa jambo muhimu wakati unapokutana na tembo. Ni bora kumkaribia tembo na upepo unaokuja kutoka kwa tembo kuja kwako.

## Cha msingi ni kutomtisha tembo

**Jaribu kufuata taratibu hizi muhimu:**

- Mkaribie tembo polepole sana.
- Wape tembo nafasi - usijaribu kuwakaribia sana.
- Epuka kushutua
  - wakati wa kutembea ni vizuri kupiga kelele (zungumza / imba) ili tembo wajue uko hapo.
- Usimkaribie tembo kwa kutokea nyuma - hawawezi kuona nyuma yao.
- Wakati inapowezekana, tengeneza sehemu kubwa ya kuzunguka kundi na uende kuwakaribia tembo kutoka pembeni au upande wa kichwani, Pia ni bora usimame na uwaache waje kwako au waondoke peke yao.

Tembo hutofautiana. Tembo wengi labda hawataki kukutana na watu, lakini tembo wengine wanaweza kwa makusudi kutaka kuumiza watu / kuharibu mali / kula mazao.

Tembo hujifunza kutokana na kukumbuka ya zamani. Ikiwa tembo amekutana na tukio baya na mtu, anaweza kuwa hatari zaidi kwa watu wengine baadaye.

Kundi la tembo jike na wadogo huwa waoga sana na huepuka makabiliano, lakini inaweza kuwa hatari sana ukiwakaribia sana.

Tembo dume wanaweza wasiwe waoga na ni ngumu kuwafukuza, lakini kutumia mbinu mbadala kama uzio wa pilipili, makopo ya bati, na uzio wa umeme itapunguza hatari.

## Tunawezaje kushiriki nafasi na tembo?

Kama watu, kuna mambo kadhaa tunaweza kufanya kujaribu kuzuia kukutana na tembo na iwe rahisi kushiriki nafasi.

- Epuka kulima au kujenga nyumba yako katika mapito ya tembo
- Heshimu mahitaji ya tembo
  - ujue njia zao ziko wapi na wapi wanaenda kunywa na kula.
- Jifunze tabia ya tembo - jua ishara za onyo